Yesu na wanyama



Sehemu za kitabu

Madondoo toka kitabu cha Gabriele,
nabii na mjumbe wa Mungu:

Hili ni Neno Langu
A na Ω
Injili ya Yesu

Ufunuo wa Kristo
unaojulikana na wakristo
halisi wa dunia nzima

(Kitabu hiki kinapatikana katika lugha ya kifaransa na ya kiingereza)

First Edition in Swahili: March 2023
1ère édition en Swahili: Mars 2023

Translated from the original German title:
Traduit de l'allemand, titre original:

Jesus und die Tiere

The German edition is the work of reference
for all questions regarding the meaning of the contents
Pour toute question se rapportant au sens,
l'édition allemande fait référence

© All Rights Reserved / Tous droits réservés
Gabriele-Verlag Das Wort GmbH

Yesu alifika katika kijiji kimoja na akamwona paka mdogo aliyetelekezwa na aliye na njaa akimkaribia huku akilia kwa sauti kubwa sana. Yesu Akamnyanyua, akamfunika kwa vazi Lake na kumwacha atulie kifuani pake.

Na alipokuwa akipita kijijini humo, akampa paka huyo chakula na kinywaji. Paka akala na kunywa na akamtolea shukrani zake. Baadaye Yesu alimkabidhi paka huyo kwa mmoja wa wanafunzi wake, mjane mmoja aliyeitwa Lorenza, aliyemhudumia paka huyo.

Kuona hivyo, watu wengine wakasema, «Mtu huyu anawahudumia wanyama wote. Je, wao ni kaka na dada zake ili Yeye awapende sana namna hiyo?» Yesu akawaambia: «Hakika viumbe hivi ni ndugu na dada zenu katika familia kubwa ya Mwenyezi Mungu, kaka na dada zenu waliopokea pumzi ya Uzima sawa na nyinyi kutoka kwa Wamilele.

Na mtu awayeyoye atakayehudumia kimoja kati ya viumbe vidogo kwa kukipa chakula na kinywaji wakati wa dhiki yake, ananifanyia Mimi. Na yule ambaye kwa makusudi atakayesababisha kwamba mmoja wao awe mhitaji, na hasiyemlinda iwapo anadhulumiwa, basi anaruhusu madhara hayo yampate kwa kisasi ambacho nilitendewa pia Mimi. Kwa sababu utatendewa katika uzima ujao, sawasawa na jinsi ulivyotenda katika uzima huu.»



Siku moja alipokuwa akitembea katika njia ya milimani pembezoni mwa jangwa, alikutana na simba aliyekuwa akiwindwa na kundi la watu huku wakimpiga kwa mawe na mikuki na kutaka kumuua.

Lakini Yesu akawakemea, akisema, «Kwa nini mnawinda viumbe wa Mungu walio na utukufu kuliko ninyi? Ni kwa sababu ya ukatili wa vizazi vingi ndiyo wamegeuka maadui

wa watu ambao wangepaswa kuwa marafiki wao.

Jinsi uwezo wa Mungu unavyoonekana ndani mwao, ndivyo uvumilivu na huruma zake vinavyoonekana. Acheni kukiwinda kiumbe hiki! Hakitaki kuwaumiza. Hamuoni jinsi simba huyu anavyowakwepa na jinsi anavyotishwa na ujeuri wenu?»

Na simba akaja kwa Yesu, akajilaza miguuni pake na kumwonyesha upendo wake. Watu walishangaa sana na kusema, «Tazama, mtu huyu anapenda viumbe vyote, na anawaamuru hata wanyama wa jangwani, nao wanamtii».



Yesu alipokuwa akitembea na wamoja wa wanafunzi wake, alikutana na mtu aliyekuwa akiwazoeza mbwa wake mawindo ya wanyama wengine. Yesu akamuambia: «Kwa nini unafanya hivyo?» Na mtu huyo akamjibu: «Ninaishi kutokana na kazi

hii. Je, wanyama hao wana manufaa gani? Wao ni dhaifu, lakini mbwa wana nguvu.»

Yesu akamwambia: «Wewe huna hekima na upendo. Elewa kwamba kila kiumbe ambacho Mungu alikiumba kina umuhimu wake. Ni nani anayeweza kueleza mema yaliyo ndani ya kiumbe hicho na kueleza kina manufaa gani kwako au kwa wanadamu?

Na kwa malisho yako: tazama mashamba jinsi yanavyomea na kutoa mazao, tazama miti jinsi ilivyojaa matunda, tazama majani! Je! Unataka nini cha ziada kuliko kazi yenye haki ya mikono yako?

Ole wenye nguvu wanaotumia vibaya nguvu zao! Ole wenye hila wanaoumiza viumbe vya Mungu! Ole kwao wawindaji! Kwa sababu wao wenyewe watawindwa.»



Siku moja Bwana aliondoka mjini na kupita milimani pamoja na wanafunzi wake. Wakafika kunako mlima wenye njia zinazo-

pita kwenye miinuko sana na wakakutana na mtu aliyekuwa na mnyama wa kubeba mizigo.

Lakini farasi alikuwa ameanguka chini kutokana na uchovu kwa sababu alikuwa amelemewa na mzigo. Mtu huyo alikuwa akimpiga farasi wake hadi kumjeruhi. Yesu akaja kwake na kumwambia: «Mwana wa ukatili, kwa nini unampiga mnyama wako? Huoni kwamba anachoka sana kwa sababu ya mzigo anaoubeba na hujui kuwa anateseka?»

Lakini mtu huyo akajibu, «Kwa nini unaingilia kati mambo yangu? Ninaweza kumpiga mnyama wangu jinsi nipendavyo, kwa sababu ni mali yangu na nilimnunua kwa kiasi kikubwa cha pesa. Waulize wale wanaosafiri nawe na wanaoishi karibu nami, wanaelewa mambo hayo.»

Na wanafunzi kadhaa wakajibu, «Ndiyo, Bwana, anachosema ni kweli, tulikuwa pale alipomnunua farasi huyo. Bwana akajibu: Hamuoni jinsi anavyovuja damu, hamsikii

kuugua kwake na malalamiko yake? Lakini wao wakajibu, «La, Bwana, hatusikii kuugua kwake wala malalamiko yake!»

Mimi, Kristo, ninaeleza, narekebisha na ninatafsiri neno kwa kina:

Hata kama mtu amenunua mnyama, mnyama huyo sio mali yake. Kama vile mwili wa kiroho yaani nafsi ndani ya mwanadamu, ni ya Uzima wa Milele kwa sababu ni Wamilele ndiye aliyeiumba. Kiumbe cha kiroho huishi na Wamilele katika Uzima wa Milele. Mnyama pia naye aliumbwa na Roho wa uumbaji wa milele, na ni wa Uzima uliopo milele na milele: yaani Mungu.

Kile kisichyo na mwisho chote ni upendo unaohudumu, Uzima unaohudumu. Mwanadamu pia anaalikwa na Mimi, Kristo, kuwatumikia jirani zake bila ubinafsi. Ni lazima tuelewe pia kwamba maneno «majirani zake» yanahusu pia majirani viumbe vingine vya mazingira, wanyama. Kwani

mnyana pia amepewa uwezo wa huduma usio na ubinafsi na anawasaidia kwa moyo mkunjufu watu wanaompenda.

Mtu asiyewapenda wenziwe bila faida hawezi kuwahudumia bila ubinafsi. Na pia mtu huyo atakuwa na tabia hiyo hiyo ya ubinafsi dhidi ya wanyama, mimea na madini.

Mnyama hasemi kwa maneno. Anateseka na kuvumilia kwa ukimya na hawezi kueleza mateso na maumivu yake. Ni yule tu anayependa viumbe wenzake, wanyama, mimea na mawe bila kulenga faida ndiye anayehisi mateso na maumivu ya mnyama.

Bwana alihuzunika na kusema: «Ole wenu ninyi ambao ugumu wa mioyo unawazuia kusikia kilio chake na dua zake kwa Muumba wake wa mbinguni. Ole mara tatu hasa kwa yule ambaye mnyama anamshtaki kuwa chanzo cha maumivu, kilio na maombolezo yake!»

Yesu akapanda na kumgusa farasi. Mnyama akasimama na majeraha yake yakapona. Lakini akamwambia mwenye farasi: «Nenda zako na usimpige tena, ikiwa wewe pia unatumaini siku moja kuonewa huruma.»



Akiwa njiani kuelekea Yeriko, Yesu alikutana na mtu aliyekuwa na njiwa na kizimba kilichojaa ndege aliowanasa. Na alitambua ukiwa na mateso yao kutokana na kupoteza uhuru wao na pia kwamba waliteseka kwa njaa na kiu.

Na akamwambia mtu huyo, «Unafanya nini na ndege hawa?» Na yule mtu akamjibu, «Ninapata riziki yangu kwa kuuza ndege ninaowanasa».

Na Yesu akamswali: «Ungeonaje iwapo mtu anayekuzidi nguvu na akili angekuchukua na kukufunga wewe au mkeo au wanao na kukutupa gerezani ili akuuze kwa faida na riziki yake?

Je, viumbe hivi si majirani wako, ila majirani walio wanyonge kuliko wewe? Na si Mungu yule yule, Baba na Mama, anayewatunza wao kama vile pia wewe? Waache huru kaka na dada zako, na usitende tena hivyo, bali jitahidi kupata mkate wako kwa njia adilifu.»

Mtu huyo akastaajabishwa na maneno ya Yesu na mamlaka yake na akawaacha huru ndege. Baada ya kutoka nje, ndege wakaruka kwa Yesu na kutua mabegani pake na kumwimbia.

Baadaye mtu huyo akamswali kuhusuu mafundisho Yake, naye akaendelea na safari yake na hatimaye akajifunza kazi ya ufumaji wa vikapu. Kutokana na kazi hiyo aliendelea kuupata mkate wake; akaharibu vizimba na mitego yake na akawa mfuasi wa Yesu.



Siku moja, Yesu alipomaliza kusema, kijana mmoja alimjia karibu na Tiberia,

mahali palipokuwa chemchemi saba, akampa sungura na njiwa walio hai ili yeye na wanafunzi wake wawale.

Yesu akamtazama kijana huyo kwa upendo na kumwambia: «Una moyo mwema na Mungu atakupa nuru; lakini hujui ya kuwa hapo mwanzo Mungu alimpa mwanadamu matunda ya nchi kwa chakula na katika hili hakumfanya kiumbe duni kuliko nyani, ng'ombe, farasi au kondoo; kwanini awaue viumbe wanaomzunguka ili ale nyama na damu yao?

Unaamini kwamba Musa aliamuru hakika viumbe hivyo vitolewe kafara na kuliwa, na ndivyo mnavyofanya hekaluni. Lakini elewa kwamba ni yule aliye na mamlaka kuliko Musa ndiye aliye hapa na anayekuja kuvunja amri ya dhabihu za damu na sherehe mbovu na kurejesha tena, kama hapo awali, sadaka safi na dhabihu zisizo za damu zinazoundwa na mbegu na matunda ya ardhi.



Yesu alienda Yerusalemu na akakutana na ngamia mwenye mzigo mzito wa kuni. Ngamia alishindwa kuufikisha mzigo kwenye kilele cha mlima, na mwenye ngamia alikuwa anampiga na kumtusi kikatili, bila ya kuweza kumsogeza mbele.

Yesu alipoona hayo, akamwambia: «Mbona unampiga ndugu yako?» Na yule mtu akasema: «Sikujua kuwa ngamia ni ndugu yangu. Je! si mnyama tu wa kubeba mizigo aliyeandaliwa kwa kunitumikia?»

Na Yesu akasema: «Je! Si huyo huyo Mungu aliyeumba kwa maada moja mnyama huyo ndiye aliyewaumba pia wanao wanaokuhudumia, na hamkupokea wote pumzi ya uhai toka Mungu?»

Mtu huyo alishangaa sana kusikia maneno hayo. Akaacha kumpiga ngamia na akampunguzia mzigo wake. Kwa hiyo ngamia akapanda kileleni, na Yesu alitembea mbele yake, na ngamia hakusimama siku nzima.

Ngamia alimtambua Yesu, kwa sababu alikuwa amehisi ndani mwake upendo wa Mungu. Na mtu huyo alitaka kujua mengi kuhusu mafundisho hayo. Yesu alimfundisha kwa hiari, naye akawa mmoja wa wafuasi wake.



Tambueni kwamba kile mnachowatendea wanyama, mnanitendea Mimi, Kristo, na pia mnazitendea nafsi zenu. Taabu na mateso ya wanyama siku moja yatakuwa pia taabu na mateso yako mwenyewe. Mungu, wa Milele, aliwakabidhi wanyama mikononi mwa mwanadamu siyo kwamba awatese bali ili aweze kuishi nao.

Wanadamu wamepewa dunia ili waweze kupata tena dhamiri kwamba wao ni wana wa Mungu, kwamba uzima wao – kama uzima wote – unatoka kwa Mungu, na ili waweze kujifunza kuthamini na kupenda

Uzima. Bila kujali umbo na kiwango cha dhamiri ambacho kinajionyesha kwa mwanadamu, Uzima, yaani – Mungu – yumo katika kila kitu.



Hakuna hata mmoja wa mitume au wafuasi Wangu aliyeamuru kuuawa kwa mwana-kondoo. Lakini kuna watu walionitolea Mimi na mitume hata pia wafuasi Wangu vipande vya nyama ya kondoo kama zawadi ya upendo. Kwa kufanya hivyo, majirani zetu hao walitaka kututolea zawadi, kwa sababu hawakuwa na ujuzi wa ubaya wa tendo hilo. Hata hivyo nilibariki zawadi hiyo na nikaanza kula nyama. Mitume na wafuasi wangu wakafanya kama Mimi. Baadaye wakaniswali swali hili: Mpaka sasa tulifikiri kwamba tunapaswa kujiepusha na lishe la nyama. Hivyo ndivyo ulivyotuamuru tufanye, lakini Wewe mwenyewe umeikula.

Hatimaye nikawaambia hivi: Mwanadamu hapaswi kuua wanyama kwa makusudi, wala kula nyama zao. Hata hivyo, wakati watu ambao bado hawajui jambo hilo wanatayarisha nyama na kumpa mwenzi wao ili kumheshimu, hapaswi kukataa zawadi hiyo. Kwani kuna tofauti kati ya kula nyama kwa pupa na kwa starehe na kuila kwa ajili ya kumshukuru mtu aliyetuandalia chakula kwa taabu aliyoipata.

Mtu aliyeandaliwa chakula na anayejua jambo hilo akiwa na uwezekano, matukio na fursa vikimruhusu, anaweza kutoa shauri la jumla kwa mhudumu wake, bila hata kujaribu kumpa somo la maadili. Baada ya muda fulani, mwenzi wetu ataelewa mwenyewe maana ya shauri hiyo ya jumla.



Kweli, nawaambieni, nimekuja ulimwenguni kuvunja dhabihu zote za damu na lishe linalotegemea nyama ya ndege au wanyama waliouawa na wanadamu.

Mimi, Kristo, ninaeleza, ninarekebisha na ninatafsiri neno kwa kina:

(...) Kuishi ndani ya Mungu hakuhusu tu uhusiano wetu na wanadamu, bali pia uhusiano na viumbe vingine kama vile wanyama, mimea, mawe na madini yote, kwa sababu kila kitu kilicho kina Uzima yaani Mungu ndani mwake. Anayeishi katika umoja na Uzima hawaui wanyama kwa hiari yake na wala haharibu mimea kwa makusudi. Anaheshimu pia Uzima – nguvu za dhamiri – za mawe na madini yote.



Mnachowatendea walio wadogo kabisa kati wana Wangu, mnanitendea Mimi. Kwa maana Mimi niko ndani mwao, nao wamo ndani Mwangu. Ndiyo, Mimi niko ndani ya viumbe vyote na viumbe vyote viko ndani Mwangu. Ninafurahi pamoja nao katika furaha zao zote na ninateseka pamoja nao katika huzuni zao zote. Ndiyo maana nawaambieni: Muwe wema wamoja kwa wengine na muwe wema kwa viumbe vyote vya Mungu.



Kwa hiyo muwe watu wenye heshima, wema, wenye huruma na wenye fadhili, si kwa wanadamu wenzenu tu, bali pia kwa viumbe vyote mlivyoagizwa kuvilinda, kwa maana katika dhiki zao ninyi ni kama miungu wanayotegemea.



Vijitabu vitolewavyo bila malipo

- Kumpata Mungu! Wapi? Na Vipi?
- Usikate tamaa! Stahimili!
- Mungu ndani mwetu
- Mafundisho ya Yesu Mlimani
- Mnaishi milele. Hakuna mauti
- Hauko peke yako
- Hili ni Neno Langu A na Ω
- Uwezekano wa kuzaliwa upya katika mwili wa mwanadamu ni neema ya Uzima





Amri Kumi za MUNGU & Mafundisho ya Yesu wa Nazareti Mlimani

Gundueni Amri Kumi za Mungu zilizofafanuliwa katika usemi wa siku hizi na pia maelezo kuhusu Mafundisho ya Yesu Mlimani iliyofunuliwa na Kristo mwenyewe kupitia Gabriele, nabii na mjumbe wa Ufalme wa milele. Ni maadili ya ulimwenguni pote isiyotegemea dini na inayomlenga kila mmoja aidhuru utamaduni wake. Jaribu mwenyewe, ikiwa inawezekana, kubadili maisha yako.

S182TBSW • ISBN 978-3-96446-289-3 • Kurasa 228

Vitabu hivi vinapatikana pia katika lugha ya kiingereza, kifaransa na nyingine nyingi pia

Infos at WhatsApp/Viber in English: +49 151 1883 8742
Infos par WhatsApp en français: +49 159 08 45 45 05
www.gabriele-publishing.com

Gabriele Publishing
The Word

Max-Braun-Straße 2 • 97828 Marktheidenfed • Germany
www.gabriele-publishing.com

